# LEARNING BY EAR

## Lent luxury - The risks of raising credit

## EPISODE THREE: THE RISK TO REPUTATION

**AUTHOR: James Muhando**

**EDITORS: Adrian Kriesch, Friederike Müller**

**PROOFREADER: Tony Dunham**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**<u>LIST OF CHARACTERS BY SCENE:</u>**

**<u>INTRO:</u>**

- **NARRATOR (M 30)**
- **COMPLAINING CUSTOMER (M ADULT)**

**<u>SCENE ONE: AT JD’S HOME, TEACHER MANDO VISITS</u>**

- **NINA (F 35)**
- **TEACHER MANDO (F 35)**
- **JD (M 15)**
- **NARRATOR (M 30)**

**<u>SCENE TWO: RIVER SABWANI</u>**

- **JENNY(F 15)**
- **JD (M 15)**
- **GIDDY (M 15)**
- **NARRATOR (M 30)**

**SCENE THREE: AT THE LOAN SHARK’S**

- **GORI (M 45)**
- **SCREAMING MAN (M ADULT)**
- **JENNY( F 15)**
- **JD (15)**
- **GIDDY (M15)**

**SCENE FOUR: ON THE WAY FROM THE LOAN SHARK’S**

- **JENNY (F 15)**
- **JD (M 15)**
- **GIDDY (M 15)**
- **NARRATOR (M 30)**

**SCENE FIVE: IN THE CITY**

- **NANCY (F 19)**
- **AIMEE (F 19)**
- **NARRATOR (M 30)**

**INTRO:**

1. **SFX:** **OFFICE AMBIENCE**
2. **SFX:** **Customer complains loudly about being denied loan while leaving**
3. **NARRATOR:**

**(Sighs)** Hujambo na kwa mara nyingine tena karibu katika mfululizo wa vipindi hivi vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako. Hii ni sehemu ya tatu katika mfuluizo wa mchezo huu, “Starehe za Kuazima-Tatizo la kugharamia Mkopo”. Ni matumaini yangu kwamba bado unakumbuka jinalangu GideonLeboo afisa anayesimamia masuala ya mikopo kwenye benki. Ama kwa hakika kazi hii ina changamoto nyingi: Mojawapo ni wakati mtu anarudi nyumbani akiwa amevunjika moyo baada ya kunyimwa mkopo, au kushtakiwa baada ya kushindwa kulipa mkopo huo! Lakini lazima uelewe kazi yangu! Na pia lazima uweze kuwaelewa watuwenye tabia mbaya, mfano mjomba Barry, wanapokuja kutafuta mkopo. Unakumbuka katika kipindi kilichotangulia, mjomba Barry alifukuzwa nyumbani baadaya kushindwa kulipa kodi? Pia unakumbuka kisa cha JD ambaye amekosa kwenda shule ili kutafuta pesa za kulipa mkopo aliochukua kununua beskeli? Maksini kijana huyo alilazimika kuzunguka usiku na mchana akitafuta pesa za kulipa mkopo huo ili wazazi wake wasijue! (laughs).

Lakini kabla ya kuendelea turudi nyuma kidogo, kuzungumzia maisha ya ujana wangu wakati nilipokuwa nikifahamika kama Giddy, na si Gideon Leboo. Tukianzia nyumbani kwa kina JD.

**SCENE ONE: AT JD'S.**

4. **SFX:** **COUNTRYSIDE AMBIENCE, UTENSILS BEING WASHED OUTSIDE.**

5. **NINA:** **(Hums)**

6. **SFX:** **FOOTSTEPS APPROACHING.**

7. **TEACHER MANDO:** Habari za asubuhi Mama JD?

8. **NINA:** **(surprised)** Mwalimu Mando karibu pita ndani!

9. **TEACHER MANDO: (Joking)** Naona unafanya usafi wa haraka, kufua nguo ! Una haraka ya kwenda wapi?

10. **NINA:** Nataka kumaliza kufua ndio nianze kukamua ng'ombe kabla giza kuingia.

11. **TEACHER:** Bora uanze na kukamuea. Siondoki bila kupata kikombe cha chai leo, tena chai ya maziwa mengi!

12. **SFX:** **THEY LAUGH.**

13. **TEACHER:** Sasa niambie! JD anaendeleaje?

14. **NINA:** Mwalimu Mando, nadhani wewe uko katika nafasi nzuri zaidi ya kufahamu vyema anavyoendelea kuliko mimi! Muda mwingi yuko shuleni!

15. **TEACHER:** Lakini sijamuona tangu muhula huu uanze.

**16. NINA:** Unasema nini?

**17. TEACHER:** Mimi nafikiri Mtoto wako ni mgonjwa, ndio sababu nimekuja kumuona!

**18. NINA:** **(Baffled)** Lakini JD huondoka hapa kila asubuhi kuja shule. Sasa sielewii unasema nini!

**19. TEACHER:** Kijana wako hajaingia darasani kwa muda wa wiki nzima sasa!

**20. NINA:** Una uhakika na unayosema, Mwalimu? Mtoto wangu hajawahi kunidanganya hata siku moja. Isitoshe amekuwa akiniambia kwamba mara nyingi analazimika kuchelewa ili kufanya kazi za shule!

**21. TEACHER:** Ninashangaa sana Mama JD. Pia mimi hajawahi kunidanganya Ma JD!

**22. SFX:** **LIGHT FOOTSTEPS ON GRASS IN BACKGROUND**

**23. NINA:** Shetani ashindwe! **(To JD)** Unataka kutoroka kwenda wapi JD? Huuuh? Rudi hapa haraka!

**24. SFX:** **FOOTSTEPS APPROACH.**

**25. NINA:** Umekuwa wapi siku zote?

**26. JD:** **SILENCE.**

**27. NINA:** Nakuuliza umekuwa wapi siku zote?

**28. JD:** **(Inaudibly)** Shuleni.

**29. NINA:** **(Aggressively)** Shule gani?

**30. JD:** Shuleni kwetu

**31. TEACHER:** Shule gani hiyo? Sijakuona kwa muda wa wiki nzima sasa!

**32. NINA:** **(angry)** Wewe unaondoka hapa kila asubuhi na vitabu, ukiwa umevalia sare za shule, kumbe kazi yako ni kushinda ukiendesha baiskeli yako! Nitakupokonya hiyo baiskeli niifungie!.Iko wapi kwanza?

**33. JD:** **(Sobbing)** Imechukuliwa na Jenny.

**34. NINA:** Kwanini ukamuachia? Wewe una tabia ya kuazima vitu vyako kwa watu wengine? Nenda haraka ukaichukue!

**35. JD:** Lakini tunatumia pamoja! Tumechangia kuinunua!

**36. NINA:** Sitaki kujua hili, nenda haraka ukailete!

**37. NARRATOR:**

Sifa ya heshima ya JD sasa imeanza kuharibika shuleni na hata nyumbani pia. Na sasa amefika kiwango cha kumpakazia rafki yake Jenny kwamba wamenunua pamoja baiskeli hiyo, huku ukweli wa mambo ni kwamba imeharibika baada ya kugongwa na lori. Je ni vipi unaweza kuepukana na hali hii? Ni kwa kudumisha heshima na ukweli!

Iwapo huwezi kugharamia kitu, hakuna haja ya kuchukua mkopo. Na ikiwa kuna lazima hiyo, basi uwe na mipango mizuri na kujua vipi utaweza kuulipa deni hilo! Lakini ni rahisi kusema kwa sababu nafanya kazi kwenye benki. Lakini pia mimi sikuwa na werevu huo kabla ya kujiunga na sekta ya benki. (**LAUGHS**).

**SCENE TWO: RIVER SABWANI**

| | | |
|---|---|---|
| **38.** | **SFX:** | **RIVER FLOWING.** |
| **39.** | **JENNY:** | Kwa hiyo umenunua baiskeli kwa mkopo JD? |
| **40.** | **JD:** | Ndio. Nimelipa nusu ya pesa hizo! Kisha zilizosalia nilipasa kuzilipa wiki liyopita. Lakini sikuweza. Sikuwa na pesa hizo. |
| **41.** | **GIDDY:** | Na sasa huna hata hiyo baiskeli unayoilipia? |
| **42.** | **JD:** | Ndio! |
| **43.** | **JENNY:** | Uko mashakani. Na ni vipi uliweza kumshawishi huyu anaitwa Suzie kukupa baiskeli kwa mkopo? |
| **44.** | **JD:** | Unajua babangu ana karakana, na amekuwa mtaja wa Suzie kwa muda mrefu. Kuna wateja wawili tu ambao Suzie anaweza kuwaamini kuwakopesha. Mumewe na babangu. |
| **45.** | **GIDDY:** | Kwa hivyo, babako alinunua baiskeli hii kwa niaba yako? |

46. **JD:** **Mmm…** naweza kusema hivyo...

47. **JENNY:** **(Not amused)** Unamaanisha nini ukisema hivyo? Hii ndio tabia ambayo imekuweka mashakani!

48. **GIDDY:** Taratibu, kuwa mpole Jenny! Wacha atueleze**. (To JD)** Unamaanisha nini, JD?

49. **JD:** **(Sighs)** Ni hivi..,nilidanganya baada ya kuwasilisha barua niliyodai kuandikwa na kutiwa sahihi na babangu, kumuomba Suzie anipe baiskeli hiyo kwa mkopo.

50. **JENNY/GIDDY:** **(Shocked)** Eti ulifanya nini?

51. **GIDDY:** Rafiki yangu! Umejiweka mashakani!

52. **JENNY:** Na ulipata wapi pesa za kulipa rehani?

53. **JD:** Kutokana na akiba yangu ya miaka miwili iliyopita! Sikutaka kurudi shuleni bila ya kuwa na baiskeli. Nilitaka kuwa kama wanafunzi wengine!

54. **JENNY:** **(Unfriendly)** Kwa hiyo unataka tukusaidie vipi? Hukutuhusisha wakati ulipokuwa ukifanya udanganyifu huo hadi kuchukua baiskeli kwa mkopo!

55. **GIDDY:** **(Calmly)** Jenny tafadhali! JD ni rafiki yetu na marafiki hufaana kwa dhiki. Tunapaswa kutafuta njia ya kumsaidia kulipa mkopo huo wa baiskeli kabla wazazi wake kujua kilichotokea.

**56. JENNY:** Vipi? Tutazipata wapi dola 60 ?

**57. PAUSE.**

**58. GIDDY:** **(Realisation)** A-ha! Nina wazo! Tunaweza kuomba mkopo kutoka kwa Gori! Yule anayeuza pesa!

**59. JENNY:** **(Shocked)** Nini ? Yule mlaghai! Siwezi!

**60. JD:** Gori?

**61. GIDDY:** Ndio Gori!. Gori si mtu mbaya kama watu wanavyodhania. Kila mara mjombangu alikuwa akikopa pesa kutoka kwake alipokuwa akiishi hapa.

**62. JENNY:** Unataka kukopa pesa tena? Yale tunayozungumzia hapa? Ni mikopo hiyo ambayo imemweka JD mashakani!

**63. GIDDY:** Pengine uniambie wazo jingine?

**64. JD:** Hapa tunajaribu kumsadia rafiki yako,.. Jenny! Naahidi sitarudia kuchukua tena mkopo!

**65. JENNY:** **(hesitates)** Unaahidi?

**66. JD:** Nakuahidi.

**67. JENNY:** Sawa. Twendeni kwa Gori!

**68. NARRATOR:**

Moja kwa moja tukaenda hadi dukani kwa Gori kutafuta mkopo. Kwa kukosa ufahamu, tukadhani tutapata mkopo huo rahisi tulivyofikiria .Lakini ..ng'o.

**SCENE THREE: AT THE LOAN SHARK'S**

***KW begin***

**69. ATMO:** **At the Loan-shark's: Interior, quiet street noise**

**70. SFX:** **PERSON DRAGGED.**

**71. GORI:** **(Angrily)** Na msirudi tena kutafuta mkopo hapa kama hamna pesa!

**72. SFX:** **KICKS & PUNCHES.**

**73. JENNY:** **(Whispers)** Twendeni !Huyu si mtu mzuri.

**74. GIDDY:** Hapana Jenny, tuzungumze naye.

**75. MAN:** **(Screams)**

***KW end***

**76. GORI:** **(Clicks his tongue, turns to them)** Mnataka nini nyinyi watoto?

**77. JENNY/JD/GIDDY: ( Timidly)** Habari bwana Gori.

**78. GORI:** Mnataka nini?

**79. JD:** Tunataka kuzungumza na wewe.

**80. GORI:** Basi semeni haraka mnachotaka! Sio kusimama tu hapo kama magogo!

**81. JD:** Tunahitaji mkopo Bw. Gori.

**82. GORI:** **(Laughs)** Nani anayetaka mkopo? Wewe?

**83. GIDDY**: Ndio sisi!

**84. GORI**: Mimi sitoi mkopo kwa kundi la watu. Nani anayetaka mkopo?

**85. JD**: Ni mimi.

**86. GORI**: Pesa ngapi?

***KW begin***

**87. GIDDY**: Dola 60 ?

**88. GORI**: Sizungumzi na wewe. Kwani ni wewe unayetaka mkopo?

**89. GIDDY**: Hapana!

**90. GORI**: Basi funga mdomo wako! Ehhe pesa ngapi?

***KW end***

**91. JD**: Dola 60.

**92. GORI**: Kwa dhamana?

**93. JD**: Dha..nini?

**94. GORI**: Dhamana. Unadhani naweze kukupa mkopo bila dhamana?

**95. JENNY**: Bw. Gori, hiyo ni kumaanisha nini?

**96. GORI**: Hujui dhamana ni nini kisha mnatafuta mkopo? Tokeni haraka hapa, na mrudi tu wakati mtakapokuwa na dhamana ya kiasi sawa na mkopo

mnaotaka wa dola 60. Dhamana ambayo nitaizuia na kuirejesha tu wakati mtakaponilipa pesa zangu. Tokeni hapa!

**97. SFX**: **HURRIED FOOTSTEPS.**

**<u>SCENE FOUR: ON THE WAY FROM THE LOAN SHARK’S.</u>**

**98. ATMO:** **COUNTRYSIDE TRAFFIC. FOOTSTEPS (3 persons)**

**99. JENNY:** Nilikuambiaje! Nilijua tu hawezi kutupa pesa!

**100. GIDDY:** Hakusema kwamba hawezi kutukopesha, amesema anataka dhamana!

**101. JENNY:** Tofauti ni nini? Lakini bado hatukupata pesa hizo.

**102. JD:** **(Worried)** Nitafanya nini sasa?

**103. GIDDY:** Sasa tufanye nini? Na ..je.. tutaweza kumletea Bw Gori hiyo dhamana hiyo,.. au sijui amepataje ?!

**104. JENNY:** Ndio ni dhamana, kwani hukua ukimsikiliza wewe mjinga? Dhamana ni kitu unachokiwasilisha au kukitoa kama hakikisho kwamba utaweza kulipa mkopo huo. Mara nyingi huwa ni kitu cha thamani sawa na mkopo unaotaka kuchukua **(pause)** Sasa tutaenda wapi, Giddy?

**105. GIDDY:** Nifuateni!

**106. NARRATOR:**

Kama kondoo wanaomfuata mchungaji wake, JD na Jenny walimfuata rafiki yao Giddy bila kuuliza maswali. Na hilo lilikuwa jambo la busara.…

***KW begin***

Kwa upande wake mjomba Barry nusra akutane na Aimee. Aliyekuwa jirani wa zamani wa mjombangu huko mashambani, kabla ya kuhamia mjini kwa masomo zaidi. Hata hivyo hawakuwa marafiki sana!

**<u>SCENE FIVE: IN THE CITY.</u>**

**107. SFX:** **CITY AMBIENCE. FOOTSTEPS.**

**108. AIMEE/NANCY: (Laugh)**

**109. NANCY:** Huko mashambani ni kuzuri sana! Nataka siku moja unipeleke nikatembee Aimee!

**110. AIMEE:** Sawa pia utapata kumfahamu Mama Kelele.

**111. AIMEE/NANCY: (LAUGH).**

**112. AIMEE:** **(Urgently)** Nancy, fanya haraka! Tuingie hapa dukani kabla yule Bwana kutuona!

**113. NANCY:** Bwana yupi?

**114. AIMEE:** Yule aliyevalia suti!

**115. NANCY:** Kwanini lakini ? Yule ni mjombako Barry?

**116. AIMEE:** Fanya haraka! Twende nitakueleza baadaye!

**117. SFX:** **QUICK FOOTSTEPS.**

**118. AIMEE:** **(Sighs)** Amenda zake! Afadhali! Anaingia Benki ya Jubilee.

**119. NANCY:** Sawa, sasa niambie, kwanini unamtoroka mjombako?

**120. AIMEE:** Si mjombangu! Ila tunatoka kijiji kimoja huko Mashambaji!

**121. NANCY:** Lakini kila mara unamuita mjomba Barry!

**122. AIMEE:** Ni kwa sababu kila mmoja anamuita hivyo!

**123. NANCY:** Lakini kwanini unamtoroka?

**124. AIMEE:** Yule Bwana ni tapeli sana! Alitoroka mashambani kwa sababu alikopa pesa kwa watu na kisha akakataa kuwalipa.

**125. NANCY:** Sasa kwanini unamtoroka? Wewe hakudai, sivyo?

**126. AIMEE:** Mimi namdai!

**127. NANCY:** Kumbe...Basi wewe ndie unayehitaji kumuona zaidi akulipe pesa zako badala ya kumtoroka !

**128. AIMEE:** Nyumba yake ilifungwa kwa sababu ya kushindwa kulipa kodi na amekuwa akiishi barabarani! Hakuna mtu anataka kumuona kwa sababu ya ukora wake.

**129. NANCY:** Kumbe! Kwa hivyo uliogopa asikuone ili asikuombe pesa tena?

**130. AIMEE:** Kuna zaidi ya hayo. Pengine angeniuliza nimruhusu kuja kuishi na mimi.

**131. NANCY:** Sasa kwanini usimkataze? Si lazima!

**132. AIMEE:** Nancy, wewe humjui mjomba Barry! Yule ana lugha tamu anaweza kumuuzia mchanga Mwarabu!

**133. NANCY:** Sawa tuachane na hayo. Twende zetu. Nataka kuingia darasani.

**134. SFX:** **FOOTSTEPS.**

**135. NARRATOR:** Unajua ni nini mjomba Barry anakwenda kufanya nini katika benki hiyo!

***KW end***

**135. SFX:** **OFFICE AMBIENCE**

**136. NARRATOR:**

Oh, mkubwa wangu ndio huyo anakuja, kwa hivyo tutaendelea na hadithi hii baadaye. Iwapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki au vingine vya Noa Bongo Jenga Maisha yako, tembelea

mtandao wetu wa dw.de/lbe. Hadi wakati mwingine kwaheri kwa sasa!